

WITO KWA WANAHISA KUFUATILIA MALIPO YA GAWIO LA MWAKA WA FEDHA 2018 & 2019

TOL Gases Limited ilikasimisha jukumu la kulipa gawio kwa wanahisa wake kwa CSD & Registry Company Limited (CSDR) kampuni tanzu ya Soko la Hisa la Dar es Salaam. Hata hivyo kufikia tarehe ya tangazo hili, bado kuna wanahisa ambao hawajachukua fedha zao za gawio la mwaka wa fedha 2018 & 2019. Na hii inatokana na CSDR kutokuwa na tarifa zao za kibenki au namba za simu ambazo zitawezesha kulipwa gawio.

Hivyo basi Mwanahisa ambaye hajalipwa gawio anapaswa kutuma taarifa za kibenki (Namba ya Akaunti na Jina la Benki), Namba ya Simu ya Mkononi pamoja na nakala ya nyaraka zifuatazo:

1. Stakabadhi ya Umiliki wa Hisa (CDS Receipt)
2. Kitambulisho (Kati ya kitambulisho cha taifa, pasi ya kusafiria, leseni ya udereva au kadi ya mpiga kura)

Mwanahisa anaweza kutuma taarifa zake kwa barua au kujaza fomu ya kuboresha kumbukumbu za Mwanahisa inayopatikana kwenye tovuti ya CSDR www.csd.co.tz na kutuma kwa Sanduku la Posta, barua pepe au whatsapp kupitia anuani ifuatayo:

Msajili wa Hisa
CSD & Registry Company Limited
Kambarage House, Gorofa ya 2, Mtaa wa Ufukoni,
S. L. P 70081
Dar es Salaam
Simu: 0746 160516/0677070414 /0685750201
Barua pepe: registrar@csdr.co.tz au nlulu@tol-gases.co.tz

**BY ORDER OF THE BOARD
TOL GASES LIMITED.**